

ASb  
approved



# Siafu Amwokoja Njiwa

Ursula Nafula


Wiehan de Jager

Kiswahili





Ilikuwa siku yenye joto jingi.



Siafu Mdogo hakuwa amepata maji kwa siku nyingi.



Akawaza, "Ninahitaji tone moja tu la maji, hata kama litatoka kwenye jani."




Umande wote ulikuwa umekauka. Hangepata hata tone moja la moja.



Siafu Mdogo akalia sana, "Nisipokunywa maji, nitakufa.  
Lazima niufikie mto nilioelezwa."




"Ati mtoni? Huko utakufa maji!" Kichakuro mmoja mwenye hekima alimwonya.



Lakini, Siafu Mdogo hakujali. Kiu chake kiliongezeka.  
"Nitakufa iwapo sitakunywa maji sasa."





Siafu Mdogo alienda kuutafuta mto alioambiwa juu yake.




Alipitia kwenye nyasi na matawi yaliyokauka.




Mara akasikia mngurumo wa mawimbi.



Siafu Mdogo alifika mtoni akayanywa maji baridi.




Alifurahi kukata kiu na hakuliona wimbi kubwa likija.



Siafu Mdogo alijaribu kujishikilia kwenye nyasi kavu zilizokuwa zikielea. Alisombwa na maji.




Siafu Mdogo alilia, "Jamani, nisaidieni."



Njiwa Mweupe alikuja akamnyooshea tawi. Akasema, "Panda juu ya tawi haraka."





Siafu Mdogo aliruka juu ya tawi na Njiwa akamwoko.



Siafu Mdogo akasema, "Siondoki kabla sijamshukuru Njiwa.  
Nitasubiri hadi atakaporejea kunywa maji."



Siku moja alipokuwa akimsubiri Njiwa, Jona na Petro walikuja mtoni. Walikuwa wamebeba manati.



"Yule Njiwa mweupe ambaye huja hapa kunywa maji, tutamla jioni." Jona akawaza.



Jona na Petro walijificha nyuma ya mimea kando ya mto.



"Sitakubali wajanja hao wamuue Njiwa. Lakini nitaifanyaje?  
Mimi ni mdogo sana." Siafu aliwaza.



Wakati huo huo Njiwa Mweupe aliruka kutoka mtini anywe maji.



Jona na Petro walipima shabaha na kungoja kwa hamu.





Siafu Mdogo alipata wazo.



Aliurukia mguu wa Petro na kumuuma.



Petro aliruka juu akalia kwa uchungu, "Waaa!" Aliyaachilia manati yake yakaanguka.



Njiwa Mweupe alishtuka akaondoka.



Hivyo ndivyo Siafu Mdogo alivyomwokoia Njiwa Mweupe.

You are free to download, copy, translate or adapt this story  
and use the illustrations as long as you attribute in the  
following way: Kholeka Mabeta and Judith Baker Author -

Kholeka Mabeta and Judith Baker

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - First sentences © African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source [www.africanstorybook.org](http://www.africanstorybook.org)

